...uwa maboresho yanayoen-

...kwanza Lugha ya Kiingereza ili wawasiliane kikamilifu na

...nguo zenye staha.

Alisema hilo linafanyika pia ikizingatiwa kuwa wato-

...vizuri sana na kuongeza kuwa, "hapa leo nimetumiwa ujumbe jinsi programu ina-

...Pia iliagiza walimu wote waingizwe kwenye utaratibu wa kufundisha kozi hiyo bila

...huo kunakuwa na madarasa yako wazi," alisema ofisa elimu huyo.

HABARI LEO UK 3.

# Ulega ang'aka wasioendeleza vitalu

**Na Anna Mwikola**

SERIKALI imeitaka Bodi na Menejimenti ya Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) kuwafukuza watu wote wanaoshindwa kuendeleza vitalu vya mifugo walivyochukua na wale wanaovikodisha kwa wengine.

Ametaka vitalu hivyo vitolewe kwa wenye mifugo na uwezo wa kuviendeleza na kuzalisha kwa tija.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, Dar es Salaam jana alipokuwa akizindua Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (Lita) na Bodi ya Utendaji ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) zilizoteuliwa hivi karibuni.

Aliitaka Bodi ya utendaji na menejimenti ya Narco kuwafukuza watu wote wanaoshindwa kuendeleza vitalu hivyo na kutaka vikodishwe kwa wenye mifugo na uwezo wa kuviendeleza na kuzalisha kwa tija.

Ulega pia aliwataka wasimamie vizuri ugawaji vitalu na kuweka viwango ili vielekezwe kwa watu wenye uwezo wa kuviendeleza badala ya kuwapa watu wanaogeuka madalali ambao huvichukua na kuvikodisha kwa wenye mifugo kwa malipo ya juu tofauti na fedha wanayolipa Narco.

"Narco wanatakiwa wapange viwango kwa wanaowapa vitalu na wajue ng'ombe wakitoka wanakwenda wapi, vitalu wapewe watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Bodi ianze kuwaondoa watu waliochukua vitalu na kuvikodisha kwa watu wenye mifugo na kisha hawalipi fedha wanazopaswa kulipa kwa Narco.

"Wafukuzeni wawekezaji walioshindwa kuendeleza uwekezaji, wapeni wengine wenye uwezo, tuache tabia kuweka watu wa kati kwenye vitalu. Msishereheshe vitu vya namna hii, mtu hana ng'ombe, hajawahi kulipa, hana uwezo wa kuendeleza, muondoeni! Wapeni watu wenye uwezo!" alisisitiza.

Ulega alimtaka Mwenyekiti wa Bodi ya Narco, Joseph Simbakalia kuhakikisha bodi yake inasimamia vema menejimenti ya Narco na kufanya uamuzi wa kiutendaji wenye tija unaoongozwa na ubunifu na mawazo mapya yatakayowezesha Ranchi za Taifa kuzalisha zaidi mazao ya mifugo hasa kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

Aliagiza Narco ihakikishe inavutia uwekezaji utakaoongeza kipato na ajira kwa Watanzania na kuwahakikishia wafugaji biashara sambamba na kuongeza uzalishaji wa nyama kufikia tani 50,000 ikiwezekana nyama ya Tanzania isafirishwe nje.

Katika hatua nyingine, Ulega aliwaeleza kuwa wana wajibu wa kuwaandalia na kuwapangia vitalu vijana waliomaliza mafunzo ya uwezeshaji vijana kwenye kilimo biashara (BBT) na wawasimamie waweze kuzalisha kwa tija.

"Narco mna kazi ya kwanza kabisa, wanaomaliza mafunzo, mjue mna wajibu wa kwenda kuwapanga kwenye vitalu na hilo lifanyike haraka, mnaanza na hao. Nikueleze Kanali mzee Simbakalia, viwanda vyetu havina malighafi, wewe na timu yako mna muda kuweka mkakati wa muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuwatumia hao vijana," alisema.

Alisema kusikia kwamba hakuna ng'ombe wa kupeleka kiwandani wakati nchi ina ranchi ni suala la aibu linalohitaji kuwekewa mkakati na si tu mkakati bali mkakati wa biashara.

Kwa upande wa Lita alimweleza Mwenyekiti wa Bodi, Mark Tsoxo kuwa wana kazi kubwa ya kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafugaji, kuwaeleza namna nzuri ya kufuga na kuwaandaa kwenda kujiajiri na kufuga kibiashara.

"Ni matarajio yangu Lita ifanye kazi ya kuwaandaa vijana wanapomaliza wasianze kutembea barabarani kutafuta kazi, waandaeni vijana kuwa tayari kupewa mitaji na kuanza kuzalisha, huo ndiyo mtazamo wetu, kwamba kila kijana ajue akitoka Lita akawe mwajiri wa kijana mwingine mmoja au zaidi," alisema.

Alisema wizara yake haiko tayari kuona Lita inafunza watu ambao baadaye wanabaki kuhangaika badala yake anataka kuona wanafunzwa kwa ajili ya kujiandaa kwenda kufanya biashara.


LEGIT AUCTION MART

**LEGIT AUCTION MART COMPANY LTD**

Dealing In: Court Process Services, Execution of Court Orders, Debt Collection and Recovery, Real Estate Agent, Tribunal Brokerage, Disposal of Public and Private Auctions etc.

**PUBLIC AUCTION**

By the order of The Resident Magistrates' Court of Dar Es Salaam at Kisutu, I shall sell by the public auction matrimonial house of the following parties.
The auction shall be held on the place, day and date as indicated in a table below;-

| S/N | EXECUTING COURT | CASE NUMBER | DECREE HOLDER VS JUDGMENT DEBTOR | PROPERTIES FOR SALE | DATE, TIME AND LOCATION FOR AUCTION |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | The Resident Magistrates' Court of Dar es Salaam at Kisutu. | Misc. Criminal Application. No. 38 of 2022 | REPUBLIC Versus STANLEY MURITHI MWAURA | Motor Vehicle Make Mitsubish Fuso Reg. No T 559 ACL, Isuzu Truck Reg. No. 167 CVV and Toyota Noah Reg. No. 796 DDT | The auction will take place on October 20th, 2023, at 10:00 a.m., in Police Barrack Ground Kurasini. |

**CONDITIONS OF SALE**

A prospective buyer will be required to deposit 25% of the auction purchase price immediately after the fall of hammer. The remaining 75% to be paid within 14 days from the date of auction, failure of which the deposited amount will be forfeited and the property resold after fresh notification.
The property may be inspected at Polisi Barrack Kurasini, Dar Es Salaam after this advertisement.

For more details please contact;
Court Broker t/a LEGIT Auction Mart Co. Ltd
Phone No; 0785 689 738
Email; legitauctionmart@gmail.com

ORD00015328

HABARI LEO UK 4

ya
ke
u,
ndani
limbali
mu za
kuwa
osha
a afua
ndo vya

ijibu wa
dadi ya
ya ma-
5/2016
a uke-
kutoka
2010 hadi
2015
mikoa
juu zaidi

ikoa hiyo
Manyara
mia 58,
doma
l-
ia nne,
usha
mia
Mara
imia 32,
imia 31

na




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akizungumza wakati wa uzinduzi wa Bodi ya 4 ya Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) uliofanyika Dar es Salaam jana. (Picha na Yusuf Badi).

M
k

Na
Ar

V

ch
Af
ar
fa
N
jiji

ki
K
ka
W
Ba
al
ka
k
Su
da
za
m

TAHARIRI /WAZO/NUKUU/MSAMIATI

HABARI LEO UK 6.

Habarileo Jumapili

# Maelekezo ya Ulega kwa Lita, Narco yazingatiwe

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, ameitaka Bodi ya utendaji na menejimenti ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) kuwafukuza watu wote wanaoshindwa kuendeleza vitalu vya mifugo.

Aidha, ametaka hatua hizo kuchukuliwa kwa wale wanaovikodisha kwa wengine na kuvitoa kwa wenye mifugo na wenye uwezo wa kuviendeleza na kuzalisha kwa tija.

Ulega alisema hayo akizindua Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (Lita) na Bodi ya Utendaji ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco) zilizoteuliwa hivi karibuni.

Taifa likiwa na ranchi nyingi zenye vitalu vya mifugo ni dhahiri kuendelea kuwa na shida katika mnyororo wa sekta ya mifugo kunakotokana na ukodishaji holela wa maeneo hayo ni lazima ukomeshwe.

Kutokana na ukweli huo tunaunga mkono agizo alilotoa Ulega kwa Bodi za Lita na Narco wa kubadilika kuwa na ubunifu na kudhibiti hali hiyo ili kuwezesha sekta hiyo kujiondoa pale ilipo na kuwa na tija kwa taifa.

Tunaamini hatua alizoelekeza Ulega ni mwanzo na msingi wa kuwa na uhakika wa uwekezaji wenye tija katika sekta ya mifugo ambayo mchango wake kwa pato la taifa bado ni mdogo.

Kama tunataka kuongeza uzalishaji wa nyama kufikia tani elfu 50 na ikiwezekana nyama ya Tanzania isafirishwe nje, vitalu vya mifugo lazima viwe kweli kwenye miliki ya wenye mifugo na sio kwa madalali ambao wanajinufaisha wao wenyewe kwa kuingiza fedha mifukoni mwao huku sekta ikiumia.

Tunapokubaliana na Ulega kuhusu kuondoa 'wapigaji hao' wanaoumiza ukuaji wa sekta ya mifugo, ugawaji upya ni lazima uelekezwe kwa wenye uwezo na katika hatua hiyo ni lazima mgawo huo uwe na viwango.

Tunasema hivyo kwa kuwa tunaamini wakipewa wenye uwezo wa kuviendeleza watawaeza pia kufanikisha programu ya kilimo biashara (BBT) kwa upande wa vijana ambao wanahitaji vitalu hivyo ili wawe na kazi za kufanya na kutumia rasilimali na ujuzi walionao kuzalisha kwa tija.

Hakika vitalu vya mifugo vina mchango mkubwa katika kunyanyua sekta hiyo hivyo kuwa katika mikono ya wababaishaji ni kuendeleza aibu ya nchi ya kukosa malighafi ya kutengenezea bidhaa za nyama wakati ina ranchi za kutosha.

Ni matumaini yetu mabadiliko katika uendeshaji wa vitalu vya mifugo kwa jinsi ilivyoelekezwa na Ulega itaendeleza ari ya kunyanyua sekta ili kuchangia kipato cha taifa na pia kutoa nafasi kwa vijana kuwa na maeneo ya kufanyia kazi katika mpango wa BBT ambapo sekta ya mifugo inapigiwa chapuo.

